

Utangamano baina ya Lugha ya Kiswahili na Lugha ya Kinyambo Kimofolojia: Uchambuzi wa Maeneo Mahususi

*Johari Hakimu*¹
Chuo Kikuu Mzumbe

DOI: <https://doi.org/10.56279/mulika.na41t1.2>

Ikisiri

Lengo la makala haya ni kuonesha utangamano wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kinyambo. Utangamano wa lugha hizo umeoneshwa katika baadhi ya vipengele vya kimofolojia ambavyo ni mbinu za uundaji wa maneno na katika utumizi wa baadhi ya viambishi. Data ya makala haya imepatikana kwa namna tofauti ambazo ni: mosi, katika orodha ya msamiati wa Kinyambo ili kupata maneno ya mkopo ya Kiswahili yanayotumika katika Kinyambo. Pili, maandiko ya wataalamu mbalimbali yamehusishwa ili kupata mifano ya maneno yenye viambishi maalumu vinavyoonesha utangamano katika lugha hizo. Tatu, ujuzi wa lugha hizi mbili alionao mwandishi wa makala haya umesaidia kupata na kuelewa data. Uchanganuzi wa data hizo umeongozwa na Nadharia ya Mofolojia Leksika ili kuonesha mipaka ya viambishi katika maneno. Uchanguzi wa data hizo umedhihirisha masuala yafuatayo: kwanza, katika uundaji wa maneno, maneno yenye vibadala vyake katika lugha ya Kinyambo yanakopwa tena kutoka Kiswahili. Hali hii imeonesha utangamano wa wazi kwa kuwa hakuna hitaji la msingi la ukopaji wa namna hiyo kutokana na kuwapo kwa vibadala vya maneno hayo katika lugha hiyo. Pili, pamoja na kwamba kuna viambishi ambavyo havikubaliki katika Kiswahili rasmi, watumiaji wa lugha ya Kiswahili wanavitumia katika mawasiliano ya kawaida. Hali hii inadhihirisha utangamano wa lugha hizo mbili kwa sababu viambishi hivyo vinatumika katika lugha zinazolingiliana sana na Kiswahili. Hivyo, kwa kuwa lugha hutangamana na kubadilika, uchambuzi wa maneno kimofolojia haupaswi kwenda mbali na mabadiliko hayo ili kuona namna maumbo ya maneno yanavyobadilika na yanavyotumika katika lugha husika ili kwenda na uhalisia ulivyo.

1.0 Utangulizi

Neno utangamano linatokana na neno tangamana lenye maana ya kuchanganyika pamoja au hali ya kushirikiana katika jumuiia (BAKITA, 2017). Hivyo, utangamano wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine unaweza kufasiliwa kama hali au mazingira ambayo baadhi ya vipengele vya lugha kama vya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, kisemantiki vinaingiliana katika lugha hizo. Kwa hiyo, makala haya yameshughulikia utangamano wa lugha ya Kiswahili na lugha ya

¹ Barua pepe: jhakimu@gmail.com

Kinyambo kimofolojia. Pamoja na kwamba lugha ya Kiswahili ni ya Kibantu, ina mazingira ya kimofolojia yanayoifananisha na kuitofautisha na lugha nyingine za Kibantu. Aidha, yapo mazingira kadhaa yanayoitangamanisha lugha hiyo na lugha nyinginezo za Kibantu kiupekee. Kwa kuwa lugha za Kibantu ni nyingi, katika makala haya imehusishwa lugha ya Kinyambo tu. Kinyambo ni lugha inayozungumzwa Kaskazini Magharibi mwa Tanzania, inayotambuliwa kwa namba E21 kwa mujibu wa mgawanyo wa lugha za Kibantu wa Guthrie (1948; 1967-71) kama anavyorejelewa na Rugemalira (2005).

Hivyo, vipengele vya kimofolojia vinavyoonesha utangamano katika lugha hizo ni pamoja na mbinu za uundaji wa maneno pamoja na utumizi wa baadhi ya viambishi. Mbinu ya uundaji wa maneno inayoonesha utangamano wa lugha hizo ni ukopaji. Dhana ya ukopaji imehusishwa katika makala haya kama kipengele cha kimofolojia. Hii ni kwa sababu wataalamu mbalimbali wa mofolojia wameitumia dhana ya ukopaji katika mofolojia kama mbinu mojawapo ya uundaji wa maneno (Lusekelo, 2014; Rubanza, 1996; Katamba, 1994). Maneno yanayokopwa na kuingizwa katika lugha nyingine hutumika pia kama kiini cha uchambuzi wa kimofolojia sambamba na maneno mengine asilia ya lugha husika. Hii ni kwa sababu mofolojia ni taaluma inayohusika na uchambuzi wa maumbo ya maneno kwa kuchunguza namna yanavyoundwa (Wesana-Chomi, 2013). Kwa hiyo, maneno ya mkopo huweza kuwa na athari katika uchambuzi wa kimofolojia wa lugha pokezi kwa sababu yanaweza kufuata mofolojia ya lugha pokezi au la na kinyume chake (taz. Hakimu, 2020). Kwa ujumla, baadhi ya maneno ya Kiswahili yanakopwa na kutumika katika lugha za Kibantu kama yalivyo au kwa kuwa na mabadiliko ya kifonolojia na/au kimofolojia. Kwa hiyo, maneno yaliyozingatiwa hapa ni yale ya Kiswahili yanayotumika katika lugha ya Kinyambo huku yakiwa na vibadala vyake na/au hayana katika lugha hiyo. Hali ya maneno hayo kuwa na vibadala inaonesha kuwa Kiswahili kina nguvu kutokana na kutumika kwake kiusambamba na/au kumeza maneno asili ya lugha husika.

Pia, utumizi wa baadhi ya viambishi unadhihirisha utangamano wa lugha hizi. Hii inatokana na baadhi ya viambishi vya lugha za Kibantu kutumika katika lugha ya Kiswahili na kuzoeleka katika baadhi ya maeneo ilhali viambishi hivyo havitumiki katika Kiswahili rasmi (Rugemalira, 2010). Uchambuzi wa viambishi hivyo unatokana na kutumika kwake katika lugha bila kujali urasmi. Wataalamu kama Hakimu (2020), Rugemalira (2010), Nurse (2007) wanaonesha viambishi vya Kibantu vinavyojitokeza katika lugha ya Kiswahili kimatumizi bila kujali urasmi wa maneno yenye viambishi hivyo. Baadhi ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili hutumia baadhi ya viambishi vinavyopatikana katika lugha nyingine za Kibantu bila kujali au kwa kutoujua urasmi wa Kiswahili. Hali hii siyo ya kupuuza au kuwalaumu wanaovitumia. Hii ni kwa sababu mara nyingi utumiaji wa maneno au viambishi katika lugha ni wa kinasibu pamoja na mazoea yaliyopo katika kutumia maneno au viambishi fulani. Kwa hiyo, hatuwezi kuishia kwenye urasmi na

usorasmi na kupuuza mabadiliko yanayojitokeza katika lugha. Mabadiliko ya lugha ni jambo lisilozuilika kutokana na sababu mbalimbali. Kutokana na sababu hizo mabadiliko ya maneno na/au viambishi kadhaa katika matumizi ni vitu vinavyopaswa kuendelea kuchunguzwa na kufanyiwa kazi. Sababu zinazochangia mabadiliko ya maneno na baadhi ya viambishi katika lugha zinaweza kuwa miongoni mwa hizi zifuatazo: kuingiliana kwa lugha, namna ya maisha, utofauti wa watu katika fikra na utambuzi, mielekeo inayohusishwa na matumizi na mabadiliko ya lugha, uchaguzi wa lugha na matokeo yake, umri na mabadiliko ya lugha, mwingiliano wa kilahaja na kimaeneo (Marshall, 2004). Hivyo, bila kuchunguza kwa kina ni sababu ipi kati ya hizo inayosababisha utangamano wa lugha hizo, makala haya yameonesha namna baadhi ya viambishi vinavyodhihirisha utangamano wa lugha kimofolojia baina ya Kiswahili na lugha ya Kinyambo.

Data iliyotumika katika makala haya imekusanywa kutoka Rugemalira (2002; 2005). Kutoka kwa Rugemalira (2002) katika orodha ya msamiati wa Kinyambo na maana zake katika Kiswahili na Kiingereza, yamepatikana maneno yaliyokopwa kutoka katika lugha ya Kiswahili na kuingia katika Kinyambo. Pia, kutoka Rugemalira (2005) imepatikana mifano ya maneno ya Kinyambo yaliyokopwa kutoka lugha ya Kiswahili. Vilevile, makala haya yamehusisha maneno yenye viambishi vinavyohitajika kwa kutumia ufahamu wa mwandishi wa lugha hizi. Sambamba na hayo, mifano iliyotumiwa katika kazi za wataalamu kama Mugaya (2019), Rugemalira (2010) na Nurse (2007) imetumika katika makala haya kama data na kwa ajili ya kushadidia maelezo na kuthibitisha utangamano wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kinyambo.

Ubainishaji wa viambishi mbalimbali vinavyodhihirisha utangamano wa lugha umetumia kiunzi cha Nadharia ya Mofolojia Leksika. Kutoka katika nadharia hiyo iliyotokana na mikabala mbalimbali (Kiparsky, 1982), umetumika mhimili mmoja tu wa kanuni ya kufuta mabano ili kuonesha mpaka na nafasi ya kila kiambishi katika maneno. Mihimili mingine ambayo haikuhusishwa katika makala haya ni pamoja na kanuni ya ngazi leksika, kanuni ya mzunguko kamili, kanuni ya ufinyu wa sifa, kanuni ya kwingineko na kanuni ya kuhifadhi muundo (Gichuru, 2010; Buberwa, 2014). Kwa hiyo, viambishi vimebainishwa kwa kuzingatia mhimili huo kwa lengo la kuonesha nafasi ya kila kiambishi. Sehemu inayofuata inaonesha utangamano wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kinyambo kimofolojia kwa kuanza na ukopaji.

2.0 Utangamano wa Kiswahili na Lugha ya Kinyambo kutokana na Ukopaji

Kama zilivyo lugha nyingine za Kibantu, lugha ya Kinyambo ina maneno ya mkopo. Maneno mengi yamekopwa kutoka katika lugha ya Kiswahili. Lugha hii ina aina mbalimbali za maneno ambazo ni nomino, viwakilishi, vivumishi, vitenzi, vielezi, viunganishi, vihusishi na viingizi/vihisishi. Katika kipengele hiki kinachohusu ukopaji, makala haya yameshughulika na aina moja ya maneno hayo ambayo ni

nomino ili kuonesha utangamano wa lugha hizi mbili. Pamoja na kwamba Rugemalila (2005) ameshughulikia mofolojia ya nomino za Kinyambo akihusisha na zile za mkopo, hakutumia nomino hizo kuonesha utangamano wa lugha hizo kimofolojia. Tofauti na Rugemalira, makala haya yameshughulikia nomino za mkopo tu. Lugha ya Kinyambo ina nomino nyingi za mkopo kutoka katika lugha ya Kiswahili kuliko aina zingine za maneno zilizotajwa hapo juu. Hii inatokana na sababu ya jumla inayosemwa na Katamba (1994) kuwa sababu ya nomino kukopwa kwa wingi siyo ngumu kuona kwani kwa kawaida neno huhitajika ili kutaja kitu kipya ambacho hakifahamiki. Kitu hicho kipya kinaweza kuwa kama mnyama au jambo la kijamii/kiutamaduni. Kwa hiyo, maneno ya Kiswahili yakishakopwa na Kinyambo yanathibitisha kuwapo kwa utangamano wa lugha hizo. Hii ni kwa sababu kama kusingekuwa na utangamano baina ya lugha hizi kusingekuwa na maneno hayo. Katika muktadha huu, utangamano huu tunaweza kuutaja kama mwingiliano wa lugha hizo unaotokana matumizi ya lugha hizo katika jamii ya Wanyambo kimiktadha. Hivyo, kwa upande mwingine, makala haya yamehusisha maneno mkopo ili kusesitiza haja ya kuchunguza kwa umakini (kimofolojia) namna yanavyojibainisha katika lugha husika.

Kutokana na maneno yaliyokopwa na Kinyambo kutoka Kiswahili, yamebainika maneno ya namna mbili: mosi, yale ya Kiswahili yanayotumika katika Kinyambo yakiwa na vibadala vyake. Pili, yanayotumika yakiwa hayana vibadala katika Kinyambo. Sehemu inayofuata inaonesha utangamano wa lugha hizo kwa kuzingatia maneno yenye vibadala na yale yasiyokuwa na vibadala.

2.1 Maneno ya Mkopo ya Kiswahili yenye Vibadala vyake katika Kinyambo

Lugha ya Kinyambo ina maneno yaliyokopwa kutoka Kiswahili ilhali yana vibadala vyake katika lugha hiyo. Ukopaji wa namna hiyo unaonesha kuwa tatizo halitokani na uhitaji wa kuwa na dhana mpya ya kutajia jambo, kitu, mnyama kama ilivyodokezwa na Katamba (1994) bali tatizo ni kwamba Kiswahili kinatumika kiusambamba au kinameza baadhi ya maneno ya lugha hiyo kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ya mwingiliano wa lugha hizo. Hii inatokana na sababu kwamba watumiaji wa Kinyambo wanaacha au wanapunguza matumizi ya maneno asilia ya lugha yao na kutumia ya Kiswahili mpaka kuzoeleka kwake. Hali hii inadhihirisha utangamano wa hali ya juu wa lugha hizo. Katika uchanganuzi wa kimofolojia wa maneno ya Kinyambo, uwapo wa maneno ya mkopo yenye vibadala vyake unapaswa kutiliwa maanani. Hii itasaidia kuona yanavyojitokeza katika lugha hiyo na kubaini mabadiliko mbalimbali ya kimofolojia. Jedwali Na. 1 linaonesha maneno ya mkopo vyenye vibadala vyake katika Kinyambo.

Jedwali Na. 1: Maneno ya Mkopo ya Kiswahili yenye Vibadala vyake katika Kinyambo

#	Maneno ya Mkopo	Vibadala katika Kinyambo	Neno la Kiswahili
1.	e-pochi (epochi)	e-nsaho (ensaho)	pochi
2.	a-mahela (amahela)	e-nsimbi (ensimbi)/e-mpia (empia)	pesa, fedha, hela
3.	e-kona/e-i-kona (ekona/eikona)	o-mukarugu (omukarugu)	kona
4.	e-amani (eamani)	Buhooro	amani
5.	i-kopo (ikopo)	o-mutaho (omutaho)	kopo
6.	e-sefuria	e-nyungu	sufuria
7.	baba	tata	baba
8.	mama	mawe	mama
9.	shangazi	tataenkazi	shangazi
10.	baba mdogo	tatento	baba mdogo

Chanzo: Data za Uwandani (2022) na Rugemalira (2002; 2005)

Mifano ya maneno katika Jedwali Na. 1 inaonesha kuwa lugha ya Kinyambo ina maneno mawilimawili yanayorejelea kitu kimoja, moja likiwa neno asilia la lugha hiyo na lingine likiwa la mkopo kutoka katika lugha ya Kiswahili. Maneno hayo yanaonesha utangamano wa lugha hizo. Sababu za utangamano huo zinaweza kuwa miongoni mwa zilizotajwa na wataalamu mbalimbali (taz. Auer (2020), Winford (2013) na Marshall (2004)).

2.2 Maneno ya Mkopo ya Kiswahili Yasiyo na Vibadala katika Kinyambo

Katika Kinyambo kuna maneno ya mkopo ya Kiswahili yasiyo na vibadala vyake katika lugha hiyo. Kuwapo kwa maneno hayo katika lugha kunakamilisha hitaji la lugha kupata dhana ya kutaja jambo/kitu jipya/kipya katika jamiilugha husika. Kutokana na maneno hayo, imebainika kuwa majina mengi yakishakopwa yanabeba viambishi kadhaa vya lugha ya Kinyambo. Viambishi hivyo ni viambishi awali tangulizi, vya ngeli na vile vinavyotokana na mabadiliko ya kimofonolojia. Pamoja na kwamba Kiswahili ni Kibantu, hakina baadhi ya viambishi vinavyopatikana katika lugha ya Kinyambo. Hii inatokana na sababu kwamba, lugha za Kibantu hutofautiana katika uebaji wa viambishi. Kiswahili, kwa mfano, hakina baadhi ya viambishi awali tangulizi katika majina na baadhi ya vitenzi tofauti na ilivyo kwa lugha nyingine za Kibantu (Katamba, 2003). Uambikaji wa viambishi hivyo unayafanya maneno yaliyokopwa katika Kiswahili na kuingia katika Kinyambo yawe kama yale ya Kinyambo. Vilevile, ukopaji wa namna hii unaonesha utangamano wa lugha hizo. Mifano ya maneno hayo katika Jedwali Na. 2 linalofuata inaonesha maneno ya namna hizo na viambishi vinavyoambikwa katika maneno hayo.

Jedwali Na. 2: Maneno ya Mkopo ya Kiswahili Yasiyo na Vibadala katika Kinyambo na Viambishi vyake

#	Maneno yenye Viambishi Mbalimbali		Neno la Kiswahili
	Umoja	Wingi	
1.	e-saa	e-saa	saa
2.	e-chikompe	e-bhikompe	kikombe/vikombe
3.	e-chitabho	e-bhitabho	kitabu/vitabu
4.	e-bhakuli	e-bhakuli	bakuli
5.	e-simu	e-simu	simu
6.	o-mukirisitu	a-bhakirisitu	Mkiristu/Wakristu
7.	o-mupaadiri	a-bhapadri	padri /mapadri
8.	e-mustaferi	a-mistafeli	mstafeli/mistafeli
9.	e-gauni	a-magauni	gauni/magauni
10.	e-kompyuta	e-kompyuta	kompyuta
11.	e-kalamu	e-kalamu	kalamu
12.	e-dafutari	a-madafutari	daftari/madaftari
13.	e-kabhata	a-makabhata	kabata/makabhata
14.	o-muzeituni	e-mizeituni	mzeituni/mizeituni
15.	o-muzabibu	e-mizabibu	mzabibu/mizabibu

Chanzo: Data ya Uwandani (2022) na Rugemalira (2002; 2005)

Kutokana na maneno yaliyomo katika Jedwali Na. 2 inaonekana kuwa maneno yaliyokopwa kutoka katika Kiswahili yana viambishi awali tangulizi ambavyo hutokea kabla ya kiambishi awali cha ngeli kinachoweza kuwa cha umoja au wingi katika nomino zenye umbo la umoja na wingi. Maneno hayo yana viambishi awali tangulizi ambavyo ni {e-} kama katika maneno *e-saa* (saa) na *e-simu* (simu) na {o-} kama katika maneno o-mupaadiri (padre) na o-muzabibu (mzabibu). Viambishi hivyo vinavyoongezeka katika maneno hayo havipatikani katika lugha ya Kiswahili kama ilivyoenezwa awali. Vilevile, maneno hayo yana viambishi awali vya umoja na wingi katika baadhi ya nomino vinavyojitokeza baada ya viambishi awali tangulizi. Baadhi ya maneno hayo yana viambishi vya ngeli vya umoja na wingi ambavyo maumbo yake yamehifadhi irabu /u/ (haikudondoshwa) katika umbo la umoja {-mu-} tofauti na lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu irabu hiyo haipo katika mifano ya maneno ya Kiswahili. Maneno hayo yana umbo {m-} tu bila irabu /u/. Kwa hiyo, umbo hili limehifadhiwa katika maneno ya Kinyambo kama mfano Na. 1 (a) na (b) unavyoonesha.

- | | |
|---|--|
| 1. (a) <i>o-mu-paadri</i>
KAT-KN(u)-MZIZI/SHINA
MZIZI/SHINA
Omupaadri
(padri) | (b) <i>o-mu-zabibu</i>
KAT-KN(u)-
omuzabibu
(mzabibu) |
|---|--|

Katika mfano Na. 1 (a) na (b) KAT inawakilisha kifupisho cha kiambishi awali tangulizi, KN(u) ni kiambishi ngeli cha umoja. Mfano Na. 1 (b) unaonesha kuwa KN(u) katika neno *omuzabibu* kina irabu /u/ ambayo katika neno la Kiswahili *mzabibu* ilishadondoshwa. Hii ina maana kuwa, kwa kuzingatia kanuni ya kimofonolojia ya udondoshaji, irabu hiyo imedondoshwa katika Kiswahili na kuhifadhiwa katika Kinyambo. Hali hii inathibitisha utangamano wa kimaumbo baina ya lugha hizi mbili kwa sababu umbo la ndani la neno *mzabibu* ni *muzabibu* katika Kiswahili hasa yakizingatiwa maumbo ya ngeli za majina. Hata hivyo, tofauti ipo katika neno *omupaadri* katika mfano Na. 1(a) kwa sababu neno hili katika Kiswahili halina kiambishi cha umoja. Neno hili ambalo katika Kinyambo lina kiambishi wa wingi {-bha-}, yaani *a-bha-paadri* (mapadri) katika Kiswahili lina kiambishi {ma-} cha wingi. Kwa hali hiyo, inaonekana kuwa lugha ya Kinyambo imejiongezea kiambishi awali cha umoja katika neno hilo ambacho hakipo katika lugha kopeshi.

Aidha, kutokana na data katika Jedwali Na. 2, inaonekana kuwa maneno ambayo hayana umoja na wingi katika lugha ya Kiswahili yanabaki kuwa na umbo hilohilo katika Kinyambo baada ya kukopwa. Maneno hayo baada ya kukopwa hubeba kiambishi awali tangulizi. Mifano ya maneno hayo ni kama inavyoonekana katika mfano Na. 2 (a) na (b)

1. (a) e-simu	(b) e-kalamu
KAT-mzizi/shina	KAT-mzizi/shina
esimu	ekalamu
(simu)	(kalamu)

Jambo la msingi la kuzingatia ni kwamba, mbali na kwamba maneno yenye umbo la umoja-wingi viambishi vyake hubadilika kutoka umoja kwenda wingi katika Kinyambo, hata KAT vyake navyo hubadilika pia kama katika maneno *e-gauni* na *a-magauni* (gauni/magauni) au *e-sefuria* na *a-masefuria* (sufuria/masufuria). Mabadiliko hayo yanayodhihirika kutokana na upachikaji wa viambishi hayapaswi kupuuzwa katika ufafanuzi wa mofolojia ya lugha ya Kinyambo.

3.0 Matumizi ya Viambishi na/au Viangami mbalimbali

Matumizi ya baadhi ya viambishi katika lugha ya Kiswahili na Kinyambo yanaonesha utangamano wa lugha hizo. Hii inatokana na sababu kwamba vipo viambishi ambavyo vinatumika katika mawasiliano yasiyo rasmi ya Kiswahili. Watumiaji wa lugha wanatumia viambishi vinavyotumika katika lugha nyingine za Kibantu katika Kiswahili katika mawasiliano yasiyo rasmi. Hii ina maana kwamba athari za Kinyambo na lugha nyinginezo za Kibantu zinadhihirika katika Kiswahili. Hata hivyo, inafahamika kuwa baadhi ya maumbo hayo yanajirejesha katika Kiswahili (Rugemalira, 2010). Hii ni kwa sababu maumbo hayo yalishakuwapo na kupotea katika Kiswahili ila kurejea kwake kumekuwapo baada ya hatua za

usanifishaji wa Kiswahili kupita. Pamoja na hayo, wataalamu kadhaa kama Rugemalira (2010), Mugaya (2019) na Hakimu (2020) wameonesha matumizi ya viambishi hivyo katika Kiswahili. Viambishi hivyo vinavyodhihirisha utangamano wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kinyambo kimofolojia vinafafanuliwa katika sehemu zinazofuata.

3.1 Kiambishi {-ag-}

Hiki ni kiambishi kinachopatikana katika nafasi ya tisa (9) katika ruwaza ya vitenzi vya Kibantu ya Meeussen (1967) akirejelewa na Nurse (2008). Nurse (2008) anaeleza kuwa katika uchambuzi wa Meeussen nafasi hiyo ina kiambishi kimoja {-ag-} na kabadala chake kikiwa {-ang-} katika baadhi ya lugha. Kiambishi hicho katika lugha ya Kiswahili hutokea kama {-ag-} kama katika maneno *enda - a-na-end-ag-a*, na *lima - tu-na-lim-ag-a*. Pamoja na hayo, kiambishi hiki kinasikika kama cha kauli ya kitenzi na katika baadhi ya lugha kimewekwa katika seti za viambishi vya kauli za vitenzi (Nurse, 2008). Pia, kiambishi hicho kina uamilifu wa kisarufi kwa kuwa kinafanya kazi kama kiambishi cha uambatizi katika kuonesha hali ya kurudia na mazoea (Nurse, 2008; Muzale, 1998 akirejelewa na Rugemalira, 2010). Kutokana na uamilifu unaobebwa na kiambishi hicho, makala haya yameshughulika na uamilifu wa kisarufi wa kiambishi hicho. Hii ni kwa sababu, katika lugha zote mbili (Kinyambo na Kiswahili) kiambishi hicho kinajitokeza kikiwa na uamilifu wa kisarufi. Vilevile, kiambishi hicho kimeshughulikiwa katika makala haya kwa sababu ndicho kinachooneshwa utangamano wa wazi baina ya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kinyambo.

Kama ilivyoielezwa awali, kiambishi hiki kinatumika katika lugha ya Kiswahili pamoja na kwamba hakitambuliki katika Kiswahili rasmi. Hii inadhihirika katika kamusi za Kiswahili kwa sababu hakuna mfano uliotolewa katika kamusi hizo ukiwa na kiambishi hicho (BAKITA, 2017; TATAKI, 2013; TATAKI, 2014). Pia, kutokana na uzoefu wa mwandishi wa makala haya wa kutumia lugha ya Kiswahili, hakuna maandiko yoyote rasmi yanayotumia maneno yenye kiambishi hicho. Kwa hiyo, watumiaji wa Kiswahili hulazimisha kutumia kiambishi hicho katika mazungumzo kunatokana na utangamano wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu zenye kiambishi hicho, ikiwamo lugha ya Kinyambo. Vilevile, mbali na kwamba kiambishi hicho hakitumiki katika Kiswahili rasmi, maelezo ya Rugemalira (2010:233) yanathibitisha matumizi ya kiambishi {-ag-} katika lugha ya Kiswahili. Rugemalira anaeleza kuwa Kiswahili rasmi kinaweza kurudisha nyuma matumizi ya kiambishi zalifu cha uambatizi {-ag-} chenye utokeaji wake mpana usiozuilika katika Kiswahili cha mazungumzo. Sambamba na hayo, Rugemalira (2010:230) anaonesha maumbo ya Kiswahili ambayo yana umbo {-ag-} ndani mwake japokuwa umbo hilo haliwezi kuchanganuliwa peke yake kama kiangami cha hali ya mazoea. Umbo hilo ni sehemu ya mzizi wa neno. Maumbo hayo ni kama *chach-ag-a* (*chachaga*), *par-ag-a* (*paraga*), na *kany-ag-a* (*kanyaga*). Maneno kama hayo yanaonesha kuwa umbo {-ag-} lipo katika lugha ya Kiswahili

pamoja na kwamba halichanganuliwi kama kiambishi kinachosimama peke yake (Hakimu, 2020). Pamoja na hayo, yapo maneno katika Kiswahili cha mazungumzo yenye kiambishi hicho kinachochanganulika. Kiambishi hicho mara nyingi hujitokeza katika vitenzi sawa na lugha nyingine za Kibantu. Kwa hiyo, mifano ifuatayo katika Jedwali Na. 2 inaonesha maneno ya Kinyambo na Kiswahili yenye kiambishi {-ag- au -ang-} chenye kuchanganulika kivyake na kina uamilifu wa kuonesha hali ya mazoea au kurudia:

Jedwali Na. 3: Maneno ya Lugha ya Kinyambo na Kiswahili yenye Kiambishi {-ag-}

Maneno ya Kinyambo yenye {-ag-}			Maneno ya Kiswahili yenye {-ag-}	
Neno	Viambishi	Maana	Neno	Viambishi
Takalimaga	ta-ka-lim-ag-a	hajawaji kulina	iliibiwaga	i-li-ib-iw-ag-a
Takagambaga	ta-ka-gamb-ag-a	hajawahi kusema	unakulaga	u-na-ku-l-ag-a
Tamwendage	Ta-mw-end-ag-e	huwa hampendi vizuri	wanapigwaga	wa-na-pig-w-ag-a
Tibhakamara ga	ti-bha-ka-mar-ag-a	hawajawahi kumaliza	anasemaga	a-na-sem-ag-a
ecitakabonwaga	e-ci-ta-ka-bhon-w-ag-a	ambacho hakijawahi kuonwa	kinasemwaga	ki-na-sem-ag-a
ecitakatemwaga	e-ci-ta-ka-tem-w-ag-a	ambacho hakijawahi kukatwa	Wanajipenda-ga	wa-ji-pend-ag-a
			Hawaheshimi-nianagi	ha-wa-heshi-mi-an-ag-i
			hatusemagi	ha-tu-sem-ag-i
			haendagi	ha-end-ag-i

Chanzo: Data ya Uwandani (2022) na Rugemalira (2010)

Kutokana na data iliyomo katika Jedwali Na. 3 hapo juu, inaonekana kuwa kiambishi {-ag-} katika lugha hizi mbili kinatokea baada ya mzizi wa kitenzi au baada ya kiambishi cha kauli za vitenzi. Kiambishi kinajitokeza baada ya mizizi kama katika neno la Kinyambo *ti-bha-ka-mar-ag-a* (tibhakamaraga) na la Kiswahili *a-na-sem-ag-a* (anasemaga) mizizi ikiwa na {-mar-} na {-sem-} mtawalia. Pia, kiambishi kinajitokeza baada ya kiambishi cha kauli ya kitenzi kama katika maneno

ya Kinyambo *e-ci-ta-ka-bon-w-ag-a* (ecitakabonwaga) na *e-ci-ta-ka-tem-w-ag-a* (ecitakatemwaga) na ya Kiswahili *i-li-ib-iw-ag-a* (ilibiwaga) na *wa-na-pig-w-ag-a*. Kiambishi hicho kimejitokeza baada ya kiambishi {-w/-iw-} cha kauli ya kitenzi kama mifano inavyoonekana. Tofauti na Kiswahili, katika Kinyambo kiambishi kinajitokeza zaidi katika ukanushi kwa mujibu wa mifano ya Rugemalira (2010) wakati katika Kiswahili kinaweza kujitokeza katika uyakinishi na ukanushi kama mifano inavyoonekana katika Jedwali Na. 3.

Pamoja na hayo, Rugemalira (2010) ameanesha namna tofauti za ubainishaji wa viambishi hivyo katika lugha hizi mbili. Namna ya kwanza ni ile ya kubainisha kiambishi {-ag-} baada ya mzizi na kiambishi cha kauli ya kitenzi na kabla ya irabu ya mwisho kama mifano inavyoonekana katika Jedwali Na. 3. Namna ya pili ni ile ya kuonesha kiambishi hiki baada ya irabu ya mwishoni mwa kitenzi kama katika neno la Kinyambo *e-ci-ta-ka-bhon-w-a-ga/e-ci-ta-ka-bhon-w-aga* (ecitakabonwaga) na katika Kiswahili *wa-na-pig-w-a-ga/wa-na-pig-aga* (wanapigwaga). Katika namna hii ya pili kiambishi hicho kinakuwa {-ga}. Uchambuzi wa namna hii unathibitisha kile kinachoelezwa na Nurse (2008) kwamba kiambishi {-ag-} kinajitokeza katika nafasi zote mbili (kabla na/au baada ya irabu ya mwishoni mwa kitenzi) katika baadhi ya lugha za Kibantu. Hivyo, utokeaji wa kiambishi hiki katika lugha ya Kiswahili unaonesha utangamano kwa kuwa kiambishi hiki hakikubaliki katika urasmi lakini watumiaji wa lugha wanakitumia katika mazungumzo yao.

3.2 Viambishi vya Umahali

Kama ilivyo kwa kiambishi {-ag-} viambishi vya umahali navyo vinaonesha utangamano baina ya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kinyambo. Hii ni kwa sababu kitendo cha viambishi hivi kuendelea kutumika katika lugha ilhali havina urasmi kinaonesha kuwa utangamano wa Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu upo na una nguvu. Kama kilivyo kiambishi {-ag-}, viambishi vya umahali siyo rasmi kwa sababu hakuna mifano iliyotolewa katika kamusi za Kiswahili huku ikiwa na viambishi hivyo (BAKITA, 2017; TATAKI, 2013; TATAKI, 2014). Pia, kutokana na uzoefu wa mwandishi wa makala haya wa kutumia lugha ya Kiswahili, hakuna maandiko yoyote rasmi yanayotumia maneno yenye viambishi hivyo vya umahali ambavyo ni {-pa-, -mu- na -ku-} katika Kiswahili. Kiambishi {-pa-} kinasimamia ngeli ukaribu kama katika tungo *hapa pana maji*. Vilevile, kiambishi {-mu-} kinasimamia umahali wa ndani ya kitu/jambo kama katika tungo *humu muna mayai*. Pia, kiambishi {-ku-} kinaonesha umahali wa mbali kama katika tungo *kule kulikuwa kunavuja*.

Hata hivyo, viambishi hivi vikijitokeza mwishoni mwa kitenzi vinakuwa {-po, -mo na -ko} kama katika vitenzi *walienda-po*, *wachezea-ko* na *aingia-mo* (Mugaya, 2019). Viambishi hivyo hujitokeza baada ya irabu ya mwishoni mwa kitenzi. Viambishi vya umahali vinavyojitokeza mwishoni kwa kitenzi ndivyo

vilivyokusudiwa katika makala haya ili kuonesha utangamano. Hii ni kwa sababu, pamoja na kwamba viambishi hivi havikubaliki katika Kiswahili rasmi, vinatumika katika mazungumzo/mawasiliano yasiyo rasmi. Hii inatokana na sababu kwamba, viambishi hivyo vinatumika kutokana na utangamano wa Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu, Kinyambo kikiwamo. Kinyambo ni miongoni mwa lugha za Kibantu zenye mofu za umahali {-ha-, -mu- na -ku-} ambazo huweza kuambikwa katika nomino. Viambishi hivyo vikiambikwa katika vitenzi vinakuwa kama viangami ambavyo vinajitokeza baada ya irabu ya mwisho kama ilivyo katika Kiswahili. Viambishi hivyo vinatokea kama {-ho-, -yo- na -mu-} kama mifano ifuatayo kutoka kwa Rugemalira (2005) inavyoonesha:

2. (a) Kiambishi/kiangami cha umahali {-ho-}

a-ha-ta-ri-**ho**

KAT-KM-UK-MZIZI-KMK

Ahatariho

(pasipokuwepo)

(b) Kiambishi/kiangami cha umahali {-yo-}

Ka-bha-ta-m-bon-a-**yo**

KAT-KI-UK-YA-MZIZI-IMM-KMK

Kabhatambonayo

(acha wasinione huko)

(c) Kiambishi/kiangami cha umahali {-mu-}

m-ta-nyw-er-a-**mu**

KI-UK-MZIZI-IM-KMK

mtanyweramu

(msinywee humu)

Kielelezo cha mifano: KAT - Kiambishi awali tangulizi

KI - Kiambishi cha kiima

KM - Kiambishi cha mahali

UK - Kiambishi cha ukanushi

YA - Kiambishi cha yambwa

IM - Irabu ya mwisho

KMK - Kiambishi cha umahali-kiangami

Mfano Na. 3 (a) - (c) unaonesha vitenzi vya Kinyambo vyenye viambishi-viangami vya umahali. Viambishi hivyo vinajitokeza baada ya nafasi ya irabu ya mwisho katika vitenzi (Rugemalira, 2005). Jambo la msingi la kuzingatia ni kwamba, viambishi vya umahali havijitokezi kwenye vitenzi vya ukanushi tu katika Kinyambo kama mfano Na. 3 (a) - (c) inavyoonesha. Viambishi hivyo vinaweza

kutumika katika vitenzi yakinishi pia kama katika mfano Na. 4 (a) - (c) inavyoonesha:

3. (a) Kiambishi/kiangami cha umahali {-ho-}

Twa-rabh-a-**ho**

KM-MZIZI-IM-**KMK**

twarabhaho

(tumepita hapo)

(b) Kiambishi/kiangami cha umahali {-yo-}

Na-rug-a-**yo**

KI-MZIZI-IM-**KMK**

narugayo

(nimetoka huko)

(c) Kiambishi/kiangami cha umahali {-mu-}

suntam-a-**mu**

MZIZI-IM-**KMK**

suntamamu

(kaa humu)

Kwa hiyo, matumizi ya viambishi hivi katika Kinyambo huleta utangamano baina ya lugha ya Kiswahili na Kinyambo. Hivyo, yawezekana Kiswahili kinavitumia nje ya urasmi kutokana na ukaribu wake na baadhi ya lugha za Kibantu. Pamoja na hayo, kama ilivyo katika Kinyambo, viambishi hivyo vya umahali vinavyojitokeza baada ya IM katika Kiswahili. Mifano ya maneno *wa-li-end-a-po* (waliendapo), *wana-cheze-a-ko* (wanachezeako) na *a-ingi-a-mo* (aingiamo) (Mugaya, 2019) inaonesha viambishi hivyo baada ya IM. Kwa ujumla, kwa namna yoyote itakavyokuwa, basi ifahamike kuwa utangamano wa lugha hizi ndio unaofanya kiambishi hiki kitumike katika Kiswahili bila kujali urasmi.

4.0 Hitimisho

Makala haya yameshughulikia utangamano wa Kiswahili na Kinyambo. Kwa kutumia maneno ya mkopo ya Kiswahili katika lugha ya Kinyambo, utangamano umedhihirika zaidi hasa kwa maneno yaliyokopwa kutoka Kiswahili na kuingia Kinyambo ilhali yana vidadala vyake katika lugha hiyo. Vilevile, utangamano umedhihirika katika viambishi vya Kibantu ambavyo havina urasmi katika Kiswahili lakini watumiaji wa lugha ya Kiswahili wanaendelea kuvitumia katika mazungumzo yao. Kwa kuwa uchunguzi wa kimofolojia hushughulikia uchambuzi na uchanganuzi wa maumbo ya maneno, ni muhimu maumbo yachunguzwe namna yalivyo na yanavyotumika katika lugha ili kubaini matumizi yake katika lugha husika. Vilevile, kwa kuwa matumizi ya lugha hubadilika, uwezekano wa viambishi hivyo kukubalika katika urasmi upo kutokana na kuendelea kutumika kwake kwa wingi na kuzoeleka katika lugha. Vipengele vichache vya kimofolojia vimehusishwa katika makala haya kwa kuwa ndivyo vinavyodhihirisha utangamano wa Kiswahili na lugha ya Kinyambo.

Marejeleo

- Auer, P. (2020) "Language Contact Pragmatic Factors". Katika E. Adamou na Y. Matras (Wah.) *The Routledge Handbook of Language Contact*. London: Routledge. Kur. 147-167. Inapatikana katika https://www.researchgate.net/publication/346912381_Language_contact. Ilisomwa tarehe 11/1/2023.
- BAKITA (2017) *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T). Limited.
- Buberwa, A. (2014) "Ruwaza za Kimofolojia za Majina ya Mahali ya Kihaya: Mtazamo wa Mofolojia Leksika". *Kiswahili*, Juz. 77(1):41-63. Inapatikana katika <https://journals.udsm.ac.tz/index.php/kiswahili/article/view/695/676>. Ilisomwa tarehe 24 Novemba 2021.
- Gichuru, T.M. (2010) Uchanganuzi wa Nomino Ambatani za Kiswahili: Mtazamo wa Mofolojia Leksia. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta. Inapatikana katika ir.library.ku.ac.ke. Ilisomwa tarehe 24 Novemba 2021.
- Hakimu, J. (2020) Ubantuishaji wa Kimofolojia katika Vitenzi vya Kiswahili vyenye Asili ya Kiarabu. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.
- Katamba, F. (1993) *Morphology*. New York: St. Martin's Press.
- Katamba, F. (1994) *English Words*. London: Routledge.
- Katamba, F. (2003) Bantu Nominal Morphology. Katika G. Nurse, D. & Philippon (Wah.), *The Bantu Languages*. USA: Taylor & Francis Routledge.
- Kiparsky, P. (1982) "Lexical Phonology and Morphology". *Encyclopedia of Language & Linguistics*, 94-97. Inapatikana katika <https://doi.org/10.1016/b0-08-044854-2/00088-2>. Ilisomwa tarehe 5 October 2021.
- Lusekelo, A. (2014) *Linguistic Morphology: A Student Guide*. Dar es Salaam: E&D Vision Publishing.
- Marshall, J. (2004) *Language Change and Sociolinguistics: Rethinking Social Networks*. New York: Palgrave Macmillan.
- Mugaya, T.S. (2019) *Mofolojia Changamani ya Kiswahili*. Dodoma: FEX Connect Publishers.
- Nurse, D. (2007) Did the Proto-Bantu verb have a Synthetic or an Analytic Structure? *SOAS Working Papers in Linguistics*. Juz. 15: 239-256.
- Nurse, D. (2008) *Tense and Aspect in Bantu*. New York: Oxford University Press.
- Rubanza, Y.I. (1996) *Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria Tanzania.
- Rugemalira, J. (2005) *Runyambo Grammar*. Dar es Salaam: Language of Tanzania Project.
- Rugemalira, J. (2010) "The -ag- TAM Marker and the Boundary between Cliticization and Affixation in Bantu". Katika K. Legere na C.T. Thorne (Wah.). *Bantu Languages: Analyses, Description and Theory*. Koln: Rudiger Koppe Verlag. kur. 229-238.
- Rugemalira, J. M. (2002) *Orunyambo: Msamiati wa Runyambo-Kiswahili-Kiingereza*. Dar es Salaam: LOT Publications.

- TUKI (2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- TUKI (2014) *Kamusi ya Kiswahili - Kiingereza (Toleo la Pili)*. Dar es Salaam: TUKI.
- Wesana-Chomi, E. (2013) *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Winford, D. (2013) "Social Factors in Contact Languages". Katika P. Bakker na Y. Matras (Wah.) *Contact Languages: A Comprehensive Guide*. Berlin: De Gruyter Mouton. kur 364-416. Imepatikana katika https://www.asc.ohio-state.edu/winford.1/docs/Social_factors_contact_langs.pdf. Iisomwa tarehe 12/1/2023.